REDET - LEAD AGENCY OF TEMCO

LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE
LHRC
KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

# MKUTANO WA KITAIFA KUHUSU UCHAGUZI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WA MWAKA 2015 ULIOANDALIWA KWA PAMOJA NA REDET NA LHRC

## TAARIFA KWA UMMA

## A. UTANGULIZI

1. Tarehe 21 Aprili 2016 ulifanyika mkutano wa kitaifa katika hoteli ya Hyatt Regency Kilimanjaro, ambao uliandaliwa na Mpango wa Utafiti na Elimu ya Demokrasia Tanzania, yaani REDET ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, LHRC, ili kujadili na kutafakari masuala muhimu yaliyotokana na uchaguzi mkuu wa 2015 kwa mtizamo wa watazamaji wa ndani wa uchaguzi.

2. Watazamaji wa ndani walijumuisha: (i) asasi za kiraia 182 chini ya mwavuli wa TEMCO zilizoongozwa na REDET; na (ii) mtandao wa asasi 17 chini ya mwavuli wa TACCEO zilizoongozwa na LHRC. Mkutano huu ulihudhuriwa na wadau wa chaguzi takriban 200 kutoka Serikalini, vyama vya siasa, watazamaji wa uchaguzi wa ndani, vyombo vya habari, asasi za kiraia, vyombo vya ulinzi na usalama, na mabalozi na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa wenye makazi yao Tanzania.

3. Mkutano ulifunguliwa na Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe (MB), Waziri wa Katiba na Sheria kwa niaba ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

4. Dhamira kuu ya mkutano ilikuwa ni kujadili na kutafakari kwa kina masuala mahsusi yaliyojitokeza wakati wa uchaguzi mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Oktoba 2015 kwa jicho la watazamaji wa ndani wa uchaguzi, TEMCO na TACCEO. Lengo kuu la mkutano lilikuwa ni kuwakutanisha wadau wa chaguzi ili kupata muafaka wa masuala muhimu yanayopaswa kuzingatiwa kutokana na mafunzo yaliyopatikana kutoka uchaguzi mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Oktoba 2015. Malengo mahsusi yalikuwa: (i) kubadilishana ujuzi, maarifa na uzoefu mintarafu uchaguzi mkuu wa 2015; (ii) kubainisha maeneo ambayo wasimamizi na wadau wa uchaguzi walifanya vizuri ili kuyadumisha na kuyaendeleza kwa manufaa ya chaguzi zijazo; (iii) kuainisha maeneo yenye upungufu na changamoto yanayotakiwa kuboreshwa kwa manufaa ya chaguzi zijazo; (iv) kutoa majumuisho, mapendekezo na ushauri kwa Serikali, vyama vya siasa, vyombo vya habari na asasi za kiraia na wadau wengine ili waangalie uwezekano wa kufanya maboresho stahiki kwa manufaa ya chaguzi zijazo.

5. Mada kuu ya mkutano ilikuwa ni **Tafakuri Kuhusu Uchaguzi Mkuu wa Tanzania, 2015: Mtizamo wa Waangalizi wa Ndani Kuelekea Chaguzi**

**za Kuaminika, Huru na Haki**. Tafakuri na mjadala vilijikita katika maeneo makubwa matano: (i) Mfumo wa kisheria na kitaasisi uliongoza uchaguzi mkuu 2015; (ii) Ushiriki wa vyama vya siasa katika uchaguzi mkuu 2015; (iii) Vyombo vya habari na makundi maalumu wakati wa uchaguzi mkuu 2015 (iv) Asasi za kiraia katika kutoa elimu ya mpiga kura na utazamaji wa uchaguzi mkuu 2015; na (v) Athari chanya na hasi zinazotokana na uchaguzi mkuu 2015.

## B. SHUKRANI

6. Washiriki wa mkutano walimshukuru kwa namna ya pekee Mgeni Rasmi Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukubali mwaliko na kwa hotuba nzuri ya ufunguzi iliyosomwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe (Mb.), Waziri wa Katiba na Sheria. Hotuba ya Mgeni Rasmi ilisheheni busara, hekima, uzalendo na uelewa mpana wa dhana ya demokrasia kwa mapana yake na uchaguzi katika muktadha wa Tanzania, nchi za Kiafrika na dunia kwa ujumla. Hotuba hiyo ilisaidia kutoa mwelekeo wa mijadala na kupanua uelewa wa washiriki. Aidha washiriki walifarijika na utayari wa Serikali ya Awamu ya Tano kuyapokea, kuyatafakari na kuyafanyia kazi mapendekezo, majumuisho na ushauri utakaotokana na mkutano.

7. Washiriki walimpongeza Mgeni Rasmi, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii inaonesha kuwa mtazamo wa Watanzania kuhusu masuala ya jinsia unazidi kuwa chanya na hii ni dalilli nzuri katika kufikia usawa wa kijinsia na uimarishaji wa demokrasia kwa ujumla.

8. Washiriki walimshukuru kwa dhati Mhe. Jaji (Mstaafu) Damian Z. Lubuva, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, na Bwana Ramadhani Kailima Mkurugenzi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Uchaguzi nchini kote kwa ushirikiano walioutoa kwa watazamaji wa ndani wa uchaguzi.

9. Mkutano ulitoa shukrani za dhati kwa Mhe. Jaji Francis Leonard Mutungi, Msajili wa Vyama vya Siasa, kwa nasaha zake nzuri kuhusu ushiriki wa vyama vya siasa katika uchaguzi mkuu wa 2015. Washiriki walimpongeza kwa kubainisha vizuri maeneo ambayo vyama vilifanya vizuri, upungufu na changamoto ambazo bado zinavikababili ili viweze kukomaa na kuwa chachu ya demokrasia nchini.

10. Washiriki kwa kauli moja walimpongeza Mzungumzaji Mkuu, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Jaji Joseph Sinde Warioba, kwa kutoa Hotuba Kuu yenye mwelekeo wa uzalendo, hekima na busara kwa mustakabali wa taifa letu. Hotuba hii ilikuwa rejea kuu katika majadiliano na ilichangia sana kutoa mwelekeo wa majumuisho, mapendekezo na ushauri kwa wasimamizi na wadau wa chaguzi. Kwa kuzingatia moyo wake wa uzalendo, utumishi uliotukuka, na mchango wake katika historia ya Tanzania washiriki walikubaliana kwamba Mhe. Jaji Warioba anastahili kuitwa "*raia aliye juu ya raia*".

11. Shukrani zilizotolewa kwa waandaaji, REDET na LHRC kwa kushirikiana kuandaa mkutano huu wa aina yake uliowakutanisha wadau wakuu wa chaguzi na washirika wa maendeleo kubadilishana mawazo na ujuzi kuhusu namna bora

ya kukidhi vigezo vya uchaguzi unaoaminika, ulio huru na wa haki mbele ya jicho la wadau wote. Washiriki walisisitiza haja ya kuendeleza ushirikiano mwema baina ya watazamaji wa ndani wa uchaguzi. Washiriki walipokea kwa furaha pongezi zilizotolewa na Mgeni Rasmi kwa waandaaji, REDET na LHRC, kwa (i) ushirikishwaji wa wadau wa chaguzi kuanzia ngazi ya mkoa hadi taifa katika kujadili na kutafakari uchaguzi wa 2015 (ii) kutumia lugha ya taifa, Kiswahili, kama lugha ya mawasiliano wakati wa Mkutano huu.

12. Mwisho, washiriki walishukuru washirika wetu wa maendeleo na kwa namna ya pekee Shirika la Misaada ya Kimataifa la Marekani, yaani USAID; Shirika la Mandeleo la Uingereza, yaani DfID; na National Democratic Institute (NDI) kwa kufanikisha maandalizi ya mkutano na kuwawezesha waangalizi wa ndani wa uchaguzi.

## C. MAJUMUISHO, MAPENDEKEZO NA USHAURI

13. Washiriki walitafakari na kujadili kwa kina masuala muhimu yaliyobainishwa katika Hotuba Kuu; majumuisho, mapendekezo na ushauri kutoka vikundi vya majadiliano mikoani; hotuba ya mgeni rasmi; na muhtasari wa uchambuzi yakinifu wa wataalam wa kila eneo kuu lilioainishwa katika kipengele cha tano.

14. Mkutano ulitafakari kwa marefu na mapana uchaguzi wa 2015 ulivyosimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia taarifa za waangalizi wa ndani na hata wa nje. Walishiriki walikubaliana na ukweli kwamba uchaguzi wa mwaka 2015 ulikuwa wa 12 baada ya uhuru na wa 14 katika historia ya miaka 58 ya chaguzi nchini. Aidha, waliafikiana na ukweli kwamba uchaguzi wa 2015 ulikuwa wa kipekee na wenye mshawasha na hamasa kubwa ikilinganishwa na chaguzi 13 zilizopita.

15. Mshawasha na hamasa hii ilitokana na mambo makuu matatu: (i) Mchakato wa Mabadiliko ya Katiba, (ii) Bunge Maalum liligawanyika katika kambi ya "UKAWA" na "Tanzania One"; na (iii) mwaka wa uchaguzi: mchakato wa uchaguzi ndani ya CCM hasa kujitokeza kwa wagombea wengi (waliochukua 42 na waliorudisha fomu za uteuzi 38) katika ngazi ya Urais, mchakato wa uteuzi ndani ya CCM, baadhi ya viongozi wa CCM kufanya "mchepuko".

16. Pamoja na kuelekeza majumuisho, mapendekezo na ushauri katika maeneo makuu matano, washiriki walielekeza kwanza tafakuri yao na mijadala kuhusu ushiriki wa wananchi, maandalizi ya Serikali na usimamizi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

17. Washiriki waliwapongeza wananchi kwa kujiandikisha, kujitokeza kupiga kura na kudumisha amani na utulivu wakati wote wa uchaguzi na baada ya uchaguzi. Mkutano ulisisitiza umuhimu wa kudumisha hali hii hata katika chaguzi zijazo.

18. Mkutano uliipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiwezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutimiza wajibu wake wa kisheria na kikatiba katika usimamizi wa uchaguzi. Aidha Serikali ilipongezwa kwa kugharamia zoezi zima la uchaguzi hususan, mchakato wa kuandikisha wapiga kura kwa kutumia mfumo wa kielektroniki, yaani BVR. Hali hii imesaidia kupunguza utegemezi na kuongeza heshima ya Serikali na Taifa.

19. Washiriki wa mkutano walivishukuru na kuvipongeza vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuhakikisha kwamba amani, usalama na utulivu unadumishwa kabla, wakati na baada ya uchaguzi. Walishauri vyombo hivi vya dola kuendelea kufanya kazi kwa weledi bila kupendelea upande wowote hususan wakati wa uchaguzi.

20. Aidha mkutano uliipongeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kwa mambo yafuatayo:
    - (i) Ugawaji wa majimbo uliofanywa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu na bila kuwa na malalamiko kutoka kwa wadau wa chaguzi;
    - (ii) Kuandikisha wapiga kura kwa wingi hadi kufikia zaidi ya asilimia 96 ya lengo lililowekwa licha ya changamoto zilizojitokeza;
    - (iii) Kushughulikia pingamizi na malalamiko yaliyotokana na uteuzi wa wagombea kwa wakati na kuyatolea maamuzi ambayo yalilinda haki za wagombea na kwa mara ya kwanza hapakuwa na mgombea ubunge aliyepita bila kupingwa;
    - (iv) Kutumia kwa ufanisi teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kurahisisha na kuboresha mawasiliano kati ya Tume na wadau wa chaguzi;
    - (v) Kutoa matokeo ya uchaguzi kwa wakati kama ilivyopangwa hususan yale ya urais; na
    - (vi) Kutoa kibali na ushirikiano wa karibu kwa watazamaji wa ndani wa uchaguzi.

21. Katika kutafakari utendaji wa Tume mkutano ulibaini kuwa utendaji wa Tume unategemea mambo makuu mawili: (i) mfumo na kisheria, hususan Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria za uchaguzi (ii) mfumo wa kitaasisi wa Tume. Walishiriki walibaini kuwa upungufu mkubwa unatokana na mfumo wa kisheria unaoongoza Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Tafakuri, majumuisho, mapendekezo na ushauri wa wajumbe wa mkutano katika maeneo mahsusi matano inafuata katika sehemu zinazofuata za taarifa hii.

**Mfumo wa kisheria na kitaasisi ulioongoza uchaguzi mkuu 2015**

22. Uchaguzi wa mwaka 2015 ulifuata mfumo wa kisheria na kitaasisi. Lakini mfumo huu una maeneo ambayo bado yanakinzana na matakwa ya uchaguzi wakuaminika, huru na haki. Baadhi ya maeneo haya yapo kwenye Katiba na sheria za nchi, ambayo ni pamoja na:

    - (i) Matokeo ya urais kutopingwa mahakamani;
    - (ii) Kutoruhusiwa kwa mgombea huru/binafsi katika nafasi zote;
    - (iii) Kukosekana kwa uwazi, ushindani na ushiriki mpana katika uteuzi wa wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi;
    - (iv) Tume kutokuwa na watumishi wanaowajibika moja kwa moja kwake katika ngazi ya mkoa, wilaya na jimbo;
    - (v) Kukosekana kwa sheria inayoruhusu vyama kuungana au kuunda umoja kwa minajili ya ushindani katika uchaguzi;
    - (vi) Kukosekana kwa sheria inayorushusu uwakilishi wa uwiano ambao ungesaidia vyama vichanga na makundi mengine katika jamii kupata nafasi katika vyombo vya uwakilishi;

(vii) Kukosekana kwa sheria inayoweka ukomo wa mwanachama kuhama kutoka chama kimoja kwenda kingine na kupewa nafasi ya kugombea;

(viii) Kukosekana kwa uwanja sawa wa ushindani baina ya vyama vya siasa kutokana na tofauti kubwa za kipato; na

(ix) Watanzania wanaoishi nje ya nchi na waliohukumiwa vifungo visivyozidi miezi sita kutoruhusiwa kushiriki katika chaguzi.

**Ushiriki wa vyama vya siasa katika uchaguzi**

23. Washiriki walivipongeza vyama vya siasa kwa kuandaa na kuhamisha wanachama wao na wanachi kwa ujumla kushiriki uchaguzi wa mwaka 2015. Pia walivipongeza vyama kwa kutovitumia vikundi vyao vya ulinzi na usalama na kuendesha kampeni ambazo kwa ujumla wake zilikuwa za kistaarabu licha ya matukio machache ya ukiukwaji wa taratibu na maadili. Hata hivyo washiriki waliainisha kasoro zilizojitokeza wakati wa uchaguzi wa mwaka 2015 ambazo ni pamoja na:

(i) Kushamiri kwa vikundi binafsi vya ulinzi na usalama wa vyama vya siasa;

(ii) Matumizi ya lugha chafu, kejeli, kebehi na matusi wakati wa kampeni;

(iii) Kuongezeka kwa vitendo vya kiubaguzi kwa misingi ya itikadi, dini, kabila, kanda, umri na jinsi;

(iv) Baadhi ya vyama kutoandaa na kunadi ilani za uchaguzi au wale waliokuwa nazo kutozitumia wakati wa kampeni na badala yake kutangaza wanachoamini wao wenyewe;

(v) Baadhi ya vyama vya siasa kutosimamisha mgombea katika nafasi yoyote ya uwakilishi;

(vi) Kuongezeka kwa vitendo vya rushwa na matumizi makubwa ya fedha kwenye uchaguzi hususan wakati wa uteuzi wa wagombea ndani ya baadhi ya vyama na kuufanya uchaguzi kununuliwa kama bidhaa;

(vii) Upungufu wa demokrasia ndani ya baadhi ya vyama vya siasa;

(viii) Kutotoa nafasi za upendeleo kwa makundi maalum katika uteuzi wa wagombea ndani ya baadhi ya vyama vya siasa; na

(ix) Baadhi ya wagombea na vyama vya siasa kushindwa kuheshimu na kutekeleza maadili ya vyama vya siasa na wagombea.

**Vyombo vya habari na makundi maalumu wakati wa uchaguzi mkuu 2015**

24. Mkutano ulivipongeza vyombo vya habari kwa kufuatilia, kuhabarisha na kuelimisha wananchi kuhusu mchakato mzima wa uchaguzi. Vilevile mkutano ulivipongeza baadhi ya vyombo vya habari kwa kuandaa vipindi maalum vya kuhamasisha ushiriki wa makundi maalum katika uchaguzi hususan kutumia lugha ya alama kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Hata hivyo washiriki wa mkutano walibainisha baadhi ya upungufu kama ifuatavyo:

(i) Vyombo vingi hasa magazeti na redio kuegemea upande mmoja na kushindwa kutoa fursa sawa kwa wagombea;

(ii) Vyombo vingi kujikita kuandika au kutangaza habari za wagombea wa urais wachache hasa wa UKAWA na CCM kuliko wengine;

(iii) Mitandao mingi ya kijamii kuandika habari zisizokuwa sahihi na kutumia lugha isiyo ya staha na hata vitisho, hali iliwachanganya na hata kuwaudhi baadhi ya wadau wa uchaguzi;

(iv) Baadhi ya vyombo vya habari kushindwa kuhseshimu na kuyaishi maadili ya uandishi wa habari na utangazaji;

(v) Baadhi ya vyombo vya habari kutoweka vipindi maalum kwa ajili ya makundi maalum; na
(vi) Wanawake wengi kutojitokeza kugombea nafasi za uongozi wa uwakilishi.

**Asasi za kiraia katika kutoa elimu ya mpiga kura na utazamaji wa uchaguzi mkuu 2015**

25. Washiriki wa mkutano walizipongeza asasi za kiraia kwa kushiriki kutoa elimu ya mpiga kura na kutazama uchaguzi. Mkutano ulibainisha kuwa, kwa ujumla, asasi za kiraia zilitimiza wajibu wake kwa Taifa. Hata hivyo, Mkutano ulibaini upungufu katika utendaji wa asasi za kiraia kama ifuatavyo:
(i) Utegemezi uliokithiri kwa wafadhili kutoka nje ya nchi;
(ii) Kushindwa kufikia maeneo yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kutoa elimu ya mpiga kura na utazamaji wa uchaguzi; na
(iii) Baadhi ya asasi za kiraia kuingiliwa na wanaharakati na hata wanasiasa na kushawishi badala ya kuelimisha.

**Athari chanya na hasi zinazotokana na uchaguzi mkuu 2015.**

26. Washiriki wa mkutano walibainisha kuwa, pamoja na harakati za kutafuta madaraka na mshawasha na hamasa za uchaguzi mkuu wa 2015, uchaguzi ulimalizika vizuri bila kulisambaratisha Taifakwani Watanzania wameendelea kuwa wamoja, kudumisha amani, mshikamano na utulivu. Aidha, mkutano ulipongeza juhudi za vyama vya siasa na wagombea kutumia vyombo vya sheria kutafuta haki pale walipohisi haki haikutendeka. Pia washiriki walipongeza hamasa iliyojitokeza miongoni mwa wananchi hususan vijana ya kudai mabadiliko.

27. Washiriki pia walitambua na kupongeza juhudi zinazofanywa na viongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano, zikiongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, za kupambana na rushwa, ufisadi na mmomonyoko wa maadili hususan katika utumishi wa umma. Aidha washiriki waliwaomba wananchi kutambua na kuunga mkono juhudi hizi za Serikali katika kujenga na kuimarisha uadilifu katika taifa letu.

28. Mkutano ulizingatia ukweli kwamba chaguzi zinahusu kinyang'anyiro na harakati za kutafuta madaraka ya kuongoza dola na rasilimali za nchi na harakati hizo zinaweza kuacha majeraha na makovu ndani ya jamii. Mkutano uliainisha athari hasi zifuatazo:

(i) Watanzania takribani milioni saba waliojiandikisha katika daftari la mpiga kura hawakujitokeza kupiga kura katika uchaguzi wa Oktoba 2015 hivyo kuleta walakini katika umakini na uelewa wao wa haki na wajibu wao kama raia wazalendo;
(ii) Baadhi ya viongozi na walezi wa kiroho kugeuka kuwa wakereketwa na wafurukutwa au mawakala wa vyama vya siasa na wagombea;
(iii) Baadhi ya vyama vya siasa na wagombea kutotambua matokeo ya uchaguzi kwa visingizio mbalimbali; na
(iv) Kuvurugika (kufutwa na kurudiwa) kwa uchaguzi wa Zanzibar.

**Mapendekezo na Ushauri**

29. Baada ya kutafakari upungufu ulioainishwa katika maeneo makuu matano, mkutano ulipendekeza hatua zinazoweza kuchukuliwa na (i) Serikali, (ii) vyama vya siasa, (iii) vyombo vya habari na (iv) asasi za kiraia.

**Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

30. Upungufu uliobainishwa katika eneo la mfumo wa kisheria na kitaasisi unaweza kufanyiwa kazi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mkutano unatambua juhudi zinazoendelea kupata katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, washiriki waliishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kukamilisha mchakato wa kupata katiba mpya ambayo itaruhusu (i) matokeo ya urais kupingwa mahakamani; (ii) mgombea huru/binafsi katika nafasi zote za uwakilishi; (iii) uwazi, ushindani na ushiriki mpana katika uteuzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na mtendaji wake mkuu; (iv) Tume ya Uchaguzi kuwa na watumishi wanaowajibika moja kwa moja kwake katika ngazi ya mkoa, wilaya na jimbo; (v) sheria kutoa mamlaka kwa Tume kusimamia chaguzi zote nchini, yaani uchaguzi mkuu na uchaguzi wa serikali za mitaa na iangalie uwezekano wa chaguzi zote kufanyika wakati mmoja; (vi) vyama vya siasa kuungana au kuunda umoja kwa minajili ya ushindani katika uchaguzi; (vii) uwakilishi wa uwiano ambao utasaidia vyama vichanga na makundi mengine katika jamii kupata viti katika vyombo vya uwakilishi; (viii) ukomo wa mwanachama kuhama kutoka chama kimoja kwenda kingine na kupewa nafasi ya ugombea; (ix) kusawazisha uwanja wa ushindani baina ya vyama vya siasa kwa kutoa ruzuku kwa vyama vyote kwa kutumia vigezo muafaka (x) Watanzania wanaoishi nje ya nchi na waliohukumiwa vifungo visivyozidi miezi sita kushiriki katika uchaguzi; (xi) vikundi binafsi vya ulinzi na usalama kutomilikiwa na vyama vya siasa; (xii) maadili ya vyama vya siasa na wagombea yapewe nguvu ya kisheria na mamlaka ya kuyasimamia; (xiii) itungwe sheria itakayowezesha uundwaji wa chombo mahsusi cha kuratibu na kusimamia utoaji wa elimu ya uraia ili kukuza na kuimarisha uzalendo na utaifa; (xiv) kuweka ukomo wa waziri kubaki madarakani katika kipindi cha kuelekea uchaguzi (xv) kitambulisho cha uraia kutumika pia kama kitambulisho cha mpiga kura.

Maboresho katika muundo wa kisheria na kitaasisi yatasaidia vyama vya siasa kujenga utamaduni wa kukubali matokeo na kuacha tabia ya kususa.

**Vyama vya siasa**

33. Upungufu uliobainishwa katika eneo la ushiriki wa vyama vya siasa unaweza kufanyiwa kazi na vyama vya siasa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mkutano unatambua juhudi zinazofanywa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa katika kuvilea, kuvielekeza na kuvishauri. Washiriki walivishauri vyama vya siasa kuzingatia yafuatayo (i) kujiepusha na vitendo vya kiubaguzi kwa misingi ya itikadi, dini, ukabila, ukanda, umri na jinsia wakati wa uchaguzi; (ii) kuandaa na kunadi ilani zao za ili kuwapa wapiga kura fursa ya kufanya uamuzi sahihi; (iii) kushiriki kikamilifu katika chaguzi kwa kusimamisha wagombea kwa kiwango kinachokubalika ama sivyo vifutiwe usajili; (iv) kusimamia kikamilifu sheria ya gharama za uchaguzi; (v) kuteua wagombea kwa kufuata misingi ya demokrasia kwa kuzingatia sheria itakayotungwa; na (vi) kutoa nafasi za upendeleo kwa makundi maalum katika uteuzi wa wagombea ndani ya vyama kwa mujibu wa sheria itakayotungwa.

**Vyombo vya habari na makundi maalum**

Mkutano ulitambua nafasi ya vyombo vya habari katika kufanikisha mchakato uchaguzi. Washiriki walionya kuwa vyombo vya habari vinaweza kuwa na athari hasi endapo vitatumika vibaya katika kipindi cha uchaguzi. Aidha, washiriki walisisitiza kuwa upungufu ulioainishwa unaweza kupunguzwa au kuondolewa kabisa kwa kuchukua hatua zifuatazo: (i) kuyapa nguvu ya kisheria maadili yanayosimamia vyombo vya habari; (ii) pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Baraza la Habari Tanzania, yaani MCT, serikali iangalie uwezekano wa kuunda chombo huru cha udhibiti wa vyombo vya habari; (iii) utafutwe utaratibu muafaka wa kuhakikisha kwamba mitandao ya kijamii inatoa habari sahihi kwa lugha ya staha, na isiyo na vitisho wala maudhi kwa wadau wa uchaguzi na wananchi kwa ujumla; na (iv) vyombo vya habari vianzishe madawati ya uchaguzi ambayo, pamoja na mambo mengine, yatazingatia mahitaji ya makundi maalum katika jamii.

**Asasi za kiraia**

34. Washiriki wa uchaguzi walitambua nafasi ya asasi za kiraia kama kiungo muhimu kati ya wananchi na viongozi wao. Aidha, walibainisha kuwa upungufu ulioainishwa katika eneo hili unaweza kurekebishwa kwa kuchukua hatua zifuatazo: (i) serikali kutenga fungu la bajeti ili kuziwezesha asasi za kiraia kutoa elimu ya uraia na mpiga kura pamoja na utazamaji wa uchaguzi; (ii) kutunga sheria itakayowezesha uundwaji wa chombo maalum cha kuratibu na kusimamia utoaji wa elimu ya mpiga kura; (iii) watazamaji wa uchaguzi kutumia njia mbalimbali kupanua maarifa na kukuza uwezo wao wa kuangalia uchaguzi ndani na nje ya nchi; na (iv) viongozi wa kiroho kujiepusha na ushabiki na uwakala wa vyama na wagombea wakati wa chaguzi.

## D. MASUALA YANAYOHITAJI MJADALA MPANA

35. Mkutano ulitafakari kwa kina mambo makuu mawili ya kitaifa ambayo hayapaswi kufumbiwa macho katika jitihada za kudumisha tunu za taifa na kuimarisha demokrasia nchini. Mambo haya ni:

(i) Hali ya siasa huko Zanzibar baada ya uchaguzi mkuu wa 2015; na,

(ii) Mchakato wa upatikanaji wa katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Washiriki wa mkutano walishauri kuwa masuala haya mawili ni nyeti kwa mustakabali wa Taifa na yanahitaji busara, hekima na muda wa kutosha wa kuyatafakari na kutafuta majawabu mujarabu.